UNOFFICIAL TRANSLATION

# Tamko la Stockholm

## Kuelekea katika makubaliano kuhusu kanuni za utungaji wa sera kwa ajili ya ulimwengu wa sasa

*Wanauchumi kumi na watatu, ambao walijumuisha Wanauchumi Wakuu wanne wa Benki ya Dunia, walikutana kwa muda wa siku mbili huko Saltsjobaden, Sweden, mnamo tarehe 16-17 Septemba 2016, kujadili changamoto zinazowakabili watunga sera za uchumi wa siku hizi. Mkutano huo ulifadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden na Benki ya Dunia. Walioshiriki katika kundi hilo ni Sabina Alkire (Oxford), Pranab Bardhan (Berkeley), Kaushik Basu (New York), Haroon Bhorat (Cape Town), Francois Bourguignon (Paris), Ashwini Deshpande (Delhi), Ravi Kanbur (Ithaca), Justin Yifu Lin (Beijing), Kalle Moene (Oslo), Jean-Philipe Platteau (Namur), Jeane Saavedra (Lima), Joseph Stiglitz (New York), na Finn Tarp (Helsinki na Copenhagen). Mwishoni mwa mkutano kikundi hiki kiliamua kutoa tamko la makubaliano yaliyofikiwa miongoni mwao: "Tamko la Stockholm".*

### 1 Changamoto ya Maendeleo

Ulimwengu leo unapitia wakati machafuko. Nguvu za dunia zinaonyesha matumaini na hatari. Maendeleo ya kiteknolojia kipekee yanaonyesha matumaini ya kuongezeka kwa viwango vya maisha, hata hivyo yanaonyesha hatari kubwa ya wafanyakazi kukosa ajira na ukosefu wa ajira kwa vijana. Upanuzi wa biashara na uwekezaji duniani umeharakisha ukuaji na kuzisogeza nchi kadhaa zenye mapato kidogo hadi hadhi ya uchumi wa kati. Wakati huohuo, vikundi vingi vya watu katika nchi hizi vimeachwa nyuma. Hali hii inatokea hata katika nchi zenye maendeleo ya kiuchumi, ambapo wengi wameathirika vibaya na nguvu za utandawazi. Zaidi ya hayo, viwango vya maisha vimeshuka sana katika mataifa ambayo yamekwama katika migogoro na vita. Kuzidi kuwepo tofauti baina ya watu ndani ya nchi kunatishia kuvuruga mshikamano wa kijamii na maendeleo ya uchumi. Uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi yanaiweka dunia hatarini, na yanahitaji kuchukua hatua za pamoja kidunia kushughulikia hatari zinazoleta matishio. Ukuaji haraka wa miji unatoa fursa ya uwezekano wa uzalishaji kutokana na watu kukusanyika pamoja – lakini pia unaweza kuongeza matatizo ya kuwepo vibanda mjini, umaskini na migogoro.

Hakuna lolote kati ya haya linalozuia maendeleo makubwa ulimwengu uliyoyaona katika ongezeko la mapato na uboreshaji wa huduma za afya na elimu. Tunasherehekea mafanikio haya, na kutazamia changamoto zisizo na shaka ambazo watunga sera watakumbana nazo. Mwitikio wenye mafanikio wa changamoto hizi unaegemea katika kutunga sera za kuongoza nguvu za dunia kwa ajili ya maendeleo na kutoa mwelekeo katika matumaini, badala ya hatari. Muundo wa sera hizo unahitaji mtazamo ulio wazi wa malengo ya sera ya maendeleo, na kujifunza kutokana na mafanikio na makosa ya siku za nyuma na kutokana na nadharia ya uchumi na uchanganuzi wa kitakwimu uliolimbikizwa kwa muda mrefu.

Sasa ni Dhahiri kuwa baadhi ya mapendekezo ya uchumi wa kimapokea yalikuwa hayafai. Watunga sera hawawezi kutegemea miongozo rahisi ya sera kama vile kukokotoa mapato ya serikali, kwa kutumia sera za fedha ili kudhibiti mfumuko wa bei, kuleta uimara wa kiuchumi, na kisha kuachia soko lifanye yaliyobaki. Kwa kuchukulia kuwa mkabala huo utaharakisha ukuaji ambao unatiririka kwenda chini hadi kwa maskini si kigezo cha kudumu. Kiuhalisia, tunakuwa na mashaka kutokana na kufuata kwa karibu ushauri wa wakati ule.

Tamko hili linaweka si mpango makini wa sera, bali seti ya kanuni ambazo tunatumaini zitasaidia katika kutunga sera ngazi ya nchi na kuendeleza mazungumzo ya kidunia na muundo wa sera za pande mbalimbali. Kanuni hizi zinazidi kuhitajika katika ulimwengu wa leo unaobadilika na kuwa wa utandawazi.

## 2 Ukuaji wa Pato la Ndani la Taifa si mwisho wenyewe

Tunaamini kuwa wakati sera za kukuza ukuaji wa Pato la Ndani la Taifa (GDP) zinahitajika, hii isiwe mwisho wenyewe bali njia ya kuunda rasilimali zinazohitajika ili kufanikisha malengo mbalimbali ya jamii, ambayo ni pamoja na kuboresha huduma za afya, elimu, ajira, usalama, na vilevile matumizi. Ustawi wa mtu mmoja mmoja ni wa viwango mbalimbali na sera inapaswa kulenga uboreshaji katika viwango vyote vinavyothaminiwa na jamii, si kipato tu. Kwa mfano, kuna haja ya kutoa lishe bora kwa watoto wa chekechea na kuhakikisha kuwa kila mmoja anapata huduma ya afya ya msingi, na kutambua kuwa haya yanakuwa ndani ya eneo la kuweza kufanyika. Iwapo hakuna sera sahihi, ukuaji wa Pato la Ndani la Taifa unaweza kuja kwa kutegemea viwango hivi vya ustawi, ikiwa ni pamoja na vile vinavyohusiana na uharibifu wa mazingira ya eneo na mabadiliko ya tabianchi duniani. Pia inafaa kukumbuka kuwa ukuaji wa Pato la Ndani la Taifa wenyewe unaweza kusababisha kukomesha tabia za uonevu na taratibu za kibaguzi dhidi ya vikundi vya watu walio katika mazingira magumu. Haya kwa kawaida yanahitaji kuchukuliwa hatua za makusudi.

Tunatambua haja ya kuelewa kuwa hakutakuwa na waraka mmoja utakaoonekana kuwa unafaa kwa aina zote za uchumi. Miktadha ya kitamaduni na kijamii inatofautiana, kama zilivyo historia. Hii inasababisha kuwa na matamanio tofauti katika jamii tofauti, na pia inachukua nafasi katika kuamua kipi kitafaa na kipi hakitafaa. Siku za nyuma kulikuwa na mwelekeo wa kuandaa msimbo mmoja wa sera inayofanana (iliyoandaliwa na nchi tajiri) kwa ajili ya mataifa yote. Ingawa kuna kanuni pana za sera sisi sote tunahitaji kuwa makini, sera inapaswa kuwa na nafasi ya uanuwai na kwenda na muktadha.

## 3 Maendeleo yanapaswa kuwa jumuishi

Tunaamini kuwa sera inapaswa kuhakikisha kuwa maendeleo ni jumuishi kijamii na kiuchumi, na hayaachi nyuma vikundi vya watu – wawe wamebainishwa kwa jinsia, kabila, au viashiria vingine vya kijamii. Inapaswa kuwa na mtazamo maalum kuhusu ukosefu wa huduma katika viwango tofauti vya ustawi, na hususan kwa watu ambao wana tatizo wanakosa huduma katika viwango vingi. Lakini msisitizo katika wale waliokosa huduma zaidi si wa kutosha. Tofauti

kati ya matajiri na maskini, na katika vikundi muhimu vya kijamii, pia ni muhimu. Ongezeko kubwa la tofauti ya kipato na utajiri iliyoshuhudiwa katika miongo ya hivi karibuni na tofauti ya viwango vya fursa iliyoonekana katika kupata huduma muhimu – kama vile huduma ya afya na elimu – kimaadili hayawezi kutetewa, yanahatarisha mshikamano wa kijamii, na kuchochea duru la kushikwa kwa sera na wasomi, jambo ambalo linaendelea kuzidisha tofauti katika jamii. Tofauti kubwa ya watu inaelekea kuwapokonya maskini sauti na hivyo kudhoofisha demokrasia. Uwezeshaji wa wanawake na vikundi vya watu waliobaguliwa kihistoria ni kipaumbele kwa haki ilivyo, lakini pia unaweka msingi unaofaa wa ufanisi wa kiuchumi. Wakati kunapokuwa na vurugu za kisiasa na mgogoro wa kijamii, maendeleo hayawezi kufanyika; na wakati sera za maendeleo zinapokuwa si jumuishi, zina uwezekano wa kuibua migogoro ya kijamii, maendeleo jumuishi ni muundo pekee wa maendeleo endelevu kijamii na kiuchumi.

## 4 Uendelevu wa kimazingira ni masharti, na si chaguo

Ingawa itasimamiwa na kutekelezwa kwa tofauti katika muktadha wa kila nchi na kanda, tunaamini kuwa utungaji wa sera ya maendeleo lazima uzingatie mazingira endelevu kama lengo kuu. Hii inahusiana moja kwa moja uharibifu wa mazingira ya mahali, ambapo ukuaji wa kipato kipekee unaweza kutoa kiashiria batili cha ustawi na maendeleo. Zaidi ya hayo, ushindani dhidi ya rasilimali na uhamaji unaohusiana na mazingira unaweza kusababisha ukosefu wa usalama na migogoro ambayo inakwamisha maendeleo. Katika ngazi ya dunia, mabadiliko ya tabianchi ni tishio la muda mrefu katika kufaa kwa sayari hii na, vilevile, tishio la muda mfupi hadi muda wa kati kwa maisha ya watu, kilimo na viumbe katika nchi nyingi. Juhudi za kukomesha uharibifu huo lazima zichukuliwe kwanza na kipekee katika ngazi ya dunia, wakati sera za kurekebisha hali hiyo zinahitaji kuingilia kati na kutoa msaada katika ngazi za kitaifa na kimaeneo. Haya ni matatizo ambayo hayawezi kuachiwa soko huria kutatua. Juhudi za usimamizi zinazofanywa na serikali na idadi fulani ya sera zinazoratibiwa nchi mbalimbali ni muhimu.

## 5 Haja ya kulinganisha masoko, serikali na jamii

Katika malengo haya na changamoto za dunia zinazoikumba jamii ya ulimwengu, sera ya maendeleo inapaswa kuzingatia ulinganifu wa busara kati ya masoko, serikali na jamii. Ni muhimu kutambua kuwa masoko yenyewe ni taasisi za kijamii ambazo zinahitaji mfumo wa usimamizi kwa ufanisi ili ziweze kutimiza ahadi yao ya kutenga kwa ufanisi rasilimali za kiuchumi. Zaidi ya hayo, hata pale ambapo masoko yanafanyika kwa ufanisi, hayana mwelekeo asilia wa kufanyika kipekee na kwa usawa. Kama tunavyojua sasa, njaa zinaendana na ufanisi wa soko huria. Mwelekeo katika masoko yasiyokuwa na vikwazo ya robo mwaka ya mwisho wa karne iliyopita yanaonyesha matokeo mbalimbali ambayo ulimwengu unaoyashuhudia sasa, ikiwa ni pamoja na matatizo ya fedha, viwango visivyotambulika vya tofauti na kutokuwa na uendelevu.

Wakati tukitambua ukomo wa yale ambayo masoko yanaweza kufanya yenyewe, tunatambua kuwa serikali yenyewe inahitaji kujiendesha kwa ufanisi. Kuna njia mbalimbali ambazo nchi zinaweza kupitiliza ufanisi masoko – kuna nafasi muhimu za kuchukuliwa na serikali katika ngazi tofauti na pia na miundo mbalimbali ambayo taasisi za kijamii zinaweza kutumia, kama vile vyama vya ushirika, umoja na AZISE. Serikali ya kitaifa inapaswa kuacha kuchukua majukumu ambayo yanafaa kuachiwa masoko au jamii. Mara kwa mara, taasisi hizi zinafanya kazi pamoja kwa kujalizana. Kuna miktadha ambapo ustawi wa wengi waliowekwa pembeni unatekelezwa kwa hatua zinazochukuliwa na vikundi vya maeneo husika katika ngazi ya jamii. Hata hivyo, hatuwezi kuacha kujali ukweli kuwa taasisi za kijamii zimetambulika kushikiliwa na nguvu zinazorudisha nyuma maendeleo, asasi za kijamii, katika ngazi zote zina nafasi muhimu katika kukuza na kudumisha mshikamano wa kijamii.

Tunarudia kusema kuwa serikali ni muhimu katika kupanga kanuni za utekelezaji na kuweka mfumo wa kisheria ambapo masoko na jamii zinaweza kustawi na kusababisha kuwepo maendeleo. Mshikamano wa kijamii unavyokuwa mkubwa zaidi na kuaminiana ndivyo kanuni bora zinavyosaidia pia zitakavyosababisha kupungua kwa tofauti za watu, vilevile ndivyo zitakavyochochea ukuaji na ustawi katika vipengele vyake vyote. Serikali pia ina nafasi muhimu katika maeneo ambapo masoko hayana ufanisi mzuri – fedha, afya na mazingira ikiwa mifano maarufu – na ambapo kuna umuhimu wa ushirikishaji, kama vile uwezeshaji wa wanawake, ulinzi wa vikundi vya watu walio pembezoni na kushughulikia utajiri uliokithiri na tofauti za vipato. Pia ina nafasi ya kuchukua katika kurekebisha sera ya viwanda na sera za kilimo na sekta za huduma zenye ufanisi. Serikali inapaswa kuzuia duru za kuongezeka kwa tofauti, zinazosababisha serikali kushikwa, ambazo kwa upande mwingine zinasimamia tofauti za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

## 6 Kuweka uimara wa uchumi wa nchi

Ushauri mwingi wa sera za kitamaduni umelenga katika haja ya kuwa na uchumi wa nchi ulio imara. Uchumi wenye uimara mkubwa hufanikiwa kwa kuwa na ukuaji mkubwa zaidi, kwa kuendeleza zaidi ustawi. Uimara wa uchumi wa nchi unamaanisha kusimamia sera ili kuuweka uchumi katika kiwango kisichoyumba na kuzingatia matokeo ya muda mrefu ya hatua za sera za sasa, hasa kwa kuhakikisha uimara wa kifedha wa ndani na nje. Nchi zinapaswa kutumia vipindi vya ukuaji imara ili kujenga rasilimali fedha ali mradi zinakuwa katika nafasi ya kutumia dawa hii wakati haja itakapotokea. Hata hivyo, ingawa nidhamu ya kifedha ya muda mrefu ni muhimu na uchumi wa kimapokea ni sahihi katika kusisitiza hili, watunga sera mara kwa mara waliishia kufanya udanganyifu wa kusawazisha bajeti.

Inabidi kutambuliwa kuwa kichocheo cha kifedha na uwekezaji wa sekta ya umma mara nyingi ni muhimu ili kuepuka mitego inayokwamisha na ni salama alimradi madeni yanasimamiwa na matokeo ya mfumuko wa bei ya uzalishaji wa fedha yanadhibitiwa. Uwekezaji wa sekta ya umma ni muhimu ili kujenga miundombinu na teknolojia ya kijani, ambapo manufaa yamesogezwa mbali sana katika siku za baadaye ili kuvutia uwekezaji wa sekta ya umma. Zaidi

ya hayo, hatua za busara zinaweza kusaidia kubadili sera ya fedha ili kuzuia maendeleo hafifu, kusimamia mzunguko duni wa mtaji na kuzuia kulimbikizana kwa madeni ya nje.

## 7 Kushughulikia athari za teknolojia ulimwenguni na tofauti zilizopo

Katika eneo la utungaji wa sera changamoto maalum imejitokeza kukiwa na maendeleo ya karibuni katika teknolojia. Teknolojia inaunganisha soko la ajira duniani, kuwezesha wafanyakazi katika nchi zinazoendelea kufanyia kazi masoko ya dunia na watumiaji bila kutakiwa kuhama wenyewe. Hii imejenga fursa mpya kwa wafanyakazi lakini wakati huo huo imezidisha tofauti ndani ya mataifa. Kuna mwelekeo wa kuongezeka katika mataifa yenye mapato makubwa kuainisha hali hii kama ajira dhidi ya tatizo la ajira, akilinganisha maslahi ya wafanyakazi katika mataifa yaliyoendelea dhidi ya maslahi ya wafanyakazi katika nchi zinazoendelea. Hii ni bahati mbaya. Kitu kinachosahauliwa ni kuwa, kwa kiasi kikubwa hili ni ajira dhidi ya tatizo la mtaji. Matumizi ya mashine zinazojiendesha, kuibuka kwa matumizi ya roboti na utandawazi wa soko la ajira si kuwa yameondoa ajira tu, bali yamechukua mapato ya wafanyakazi kukiwa na faida kubwa kwa mashirika na wamiliki wa mashine. Matokeo haya ni tatizo ambalo linapaswa kushughulikiwa bila kubadili hii kuwa ajira dhidi ya mapambano ya ajira duniani.

Hii inaweka masharti matatu ya ajira. Kwanza, tunapaswa kuwekeza katika mtaji wa binadamu na kuongeza ujuzi kwa njia ambazo zinaweza kujazia teknolojia na hatimaye kuongeza kipato cha ajira, pamoja na kuongezeka kwa teknolojia. Pili, tunapaswa kutunga sheria mpya za uhamishaji wa mapato ndani ya mataifa. Kushuka kwa kiasi cha ujira katika Jumla ya Pato la Ndani hakutakiwi kuchukuliwa kama matokeo yasiyoepukika ya kuibuka kwa teknolojia. Serikali zinapaswa kujenga mifumo ya kodi na kugawana faida ili kuweka uwiano huu, na zinapaswa kuweka utaratibu wa zoezi hili – kama vile usimamizi madhubuti wa sheria za ushindani na sheria ya ajira – ambazo zinawawezesha wafanyakazi kuwa na uwezo wa kujadiliana na kuwapatia sauti zaidi katika jamii na ndani ya makampuni. Hatimaye, hii inafanya kuwepo mahitaji maalum ya nchi mbalimbali kutunga sera za pamoja. Hii inaweka wajibu kwa taasisi zilizowekeza katika nchi mbalimbali kuhimiza ulinganishaji wa sera miongoni mwa mataifa na kukuza sera ambazo zinazingatia maslahi si ya mataifa tajiri, yenye viwanda tu, bali pia ya nchi zinazoibukia kiuchumi, ambazo mara nyingi zinakuwa zimenyimwa sauti katika utoaji wa maamuzi kimataifa.

## 8 Kanuni za kijamii na masuala ya mitazamo

Sehemu kubwa ya uchumi wa kimapokeo umechukulia kanuni za kijamii na mitazamo kuwa na athari kidogo katika maisha yetu ya kiuchumi. Ongezeko kubwa la kazi za utafiti linaonyesha kuwa hali haiko hivyo. Maadili na utamaduni wetu si kuwa ni muhimu yenyewe, pia yanaathiri namna uchumi unavyofanyika. Jamii ambapo watu wanaaminiana inafanya vizuri zaidi kuliko pale ambapo hawaaminiani. Vilevile seti ya chaguzi, wakati inapowasilishwa kwa njia tofauti kwa watu, kwa mfano, kwa mpangilio tofauti au kwa

mpangilio tofauti wa chaguzi, inaweza kuleta tofauti ya chaguzi za watu watakazofanya. Serikali zinapaswa kuanza kutumia mitazamo hii mipya na sheria mpya ili kuendesha programu na huduma zao kwa ufanisi zaidi. Kampuni na mashirika ya sekta binafsi yamekuwa kwa muda mrefu yakitumia na kuendeleza mara kwa mara maarifa yao ya saikolojia ya binadamu na upendeleo wa kijamii kuendeleza maslahi na faida zao. Iwapo serikali zinahitaji kutoa huduma ya elimu na afya kwa ufanisi na kukusanya kodi kwa haki, uelewa wetu wa kanuni za kijamii unapaswa kuwekwa katika kutunga sera kwa nia njema. Kanuni za kijamii na mitazamo pia inaweza kuchukua nafasi muhimu katika kupambana na rushwa. Hili ni eneo moja ambapo muktadha maalum wa mataifa ni muhimu, kwa kuwa kanuni na mitazamo ni bidhaa za historia na uzoefu wa kila jamii.

## 9 Sera za dunia na wajibu wa jamii ya kimataifa

Nguvu za dunia zinazidi kutunga sera za njia za maendeleo kwa uwazi kwa serikali za kitaifa. Zinawasilisha vikwazo na fursa na zenyewe kwa upande mwingine, zinaamuliwa na vitendo vya nchi nyingine.

Sera ya fedha katika mataifa yenye mapato makubwa zinaathiri maendeleo ya mtiririko wa mtaji kwenda nchi zinazoendelea. Sera za usimamizi wa fedha katika nchi tajiri, ingawa katika hatua ya kwanza zinaathiri nchi hizi, hatimaye zinakuwa na athari katika uchumi unaoibukia na unaoendelea, kama ilivyoonyeshwa vya kutosha na matatizo ya kifedha mwaka 2008. Sera na kanuni kuhusu msamaha wa kodi zinaathiri uwezo wa nchi zote, na hususan nchi zenye mapato kidogo, kukusanya mapato ya kulipia sera zao kwa ajili ya maendeleo jumuishi na endelevu. Sera za biashara za taifa moja zinaathiri maendeleo ya usafirishaji bidhaa nje ya nchi ya taifa jingine. Sera za uhamiaji katika nchi zenye mapato makubwa zinaathiri uwezekano wa wananchi wa nchi zenye mapato kidogo kufanya vizuri wenyewe na kwa kufanya hivyo kupitia usafirishaji wa fedha na uhamishaji wa maarifa, husaidia maendeleo ya nchi zao wanakotoka. Kwa hali kama hii, kila nchi katika ulimwengu wa leo wa utandawazi ina athari ya ziada kwa nyingine. Kwa hali hii, nchi zote zina wajibu wa kuzingatia na kuendeleza fursa za maendeleo kwa wananchi wa ulimwengu walionyimwa haki.

Makubaliano na taasisi ambazo zinafanya kazi katika nchi nyingi ni muhimu katika kushughulikia baadhi ya matatizo makubwa zaidi ya wakati wetu. Hata hivyo, haya ni makubaliano na taasisi ambazo zinaonekana kuwa ngumu zaidi kuanzisha na kudumisha. Ingawa Makubaliano ya Paris kuhusu mabadiliko ya tabianchi yanawakilisha mwanzo mzuri, ulimwengu unasubiri utekelezaji wa ahadi kuhusu uzalishaji wa hewa ya ukaa utakaofanywa na nchi zote, na utoaji wa misaada unaofanywa na nchi zenye mapato makubwa kwa ajili ya juhudi za kuleta mabadiliko ya tabianchi – kukomesha na kupitisha – kunakofanywa na nchi zenye mapato kidogo. Miaka ya hivi karibuni imeshuhudia kupungua kwa misaada ya maendeleo kutoka vyanzo vya kawaida na kuenea kwa taasisi mpya za maendeleo za pande mbili na zinazofanya kazi katika nchi mbalimbali, ukiacha lengo telezi la kufikia 0.7% ya lengo kwa msaada rasmi wa maendeleo lililokubaliwa na nchi za ulimwengu muongo mmoja uliopita. Jamii ya kimataifa ina wajibu wa kuhakikisha kuwa msaada unaelekezwa katika nchi

zinazoendelea, na vikundi vya watu walioachwa pembezoni baina yao, na kuwa nchi zinazoendelea ziwakilishwe vizuri katika vyombo vya utawala vya taasisi za kimataifa, hali ambayo kwa upande mwingine itahakikisha kuwa mikataba na makubaliano ya kimataifa yanajali mahitaji ya nchi zinazoendelea.

## 10 Matarajio

Iwapo nchi zitafuata sera kwa vitendo za kulinganisha masoko, dola na jamii katika kushughulikia changamoto za maendeleo, na iwapo jamii ya kimataifa itafanya kazi kwa pamoja kuondoa vikwazo vya nguvu za dunia na kutumia fursa mpya zinazotolewa, maendeleo ya kiteknolojia ulimwengu unayoyapata yanaweza kutafsiriwa kuwa maendeleo katika ustawi wa wote, ikiwa ni pamoja na wale walionyimwa haki. Tunaweza kufanikiwa kuwa na ulimwengu wenye ustawi wa pamoja. Makosa na mafanikio ya siku za nyuma yanapendekeza seti ya kanuni ambapo sera hizo katika ngazi ya kitaifa na kidunia zinaweza kutungwa. Sasa ni wakati wa kutumia kanuni hizi kiutaratibu katika kubuni sera za uchumi kwa maendeleo.